

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**

Anwani ya Simu: "TUME"  
DODOMA  
Namba ya Simu: 0738166703  
0733005974



Tume ya Utumishi wa Umma,  
Jengo la Chimwaga,  
Ghorofa ya 2,  
2 Barabara ya UDOM,  
S.L.P. 1074,  
**40405 DODOMA.**

*Barua pepe:*

[secretary@psc.go.tz](mailto:secretary@psc.go.tz)

*Tovuti:* [www.psc.go.tz](http://www.psc.go.tz)

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Jaji (Mstaafu) Hamisa Hamis Kalombola anatarajia kuongoza Mkutano wa Tume Na. 02 kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 utakaofanyika Jijini Dodoma, kuanzia tarehe 20 Juni 2022 hadi tarehe 08 Julai 2022.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) (d) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 [Marejeo ya mwaka 2019], Tume ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kupokea na kushughulikia Rufaa za mashauri yaliyotolewa maamuzi na Mamlaka za Nidhamu.

Tume katika mkutano huu, itapokea, kujadili na kutolea uamuzi Rufaa na Malalamiko mbalimbali yaliyowasilishwa Tume na Watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na Uamuzi uliotolewa na Waajiri, Mamlaka za Ajira na Mamlaka zao za Nidhamu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma, Bw. Mathew M. Kirama, shughuli nyingine zilizopangwa kufanyika wakati wa Mkutano ni kupitia taarifa mbalimbali za utendaji wa Tume.

Imetolewa na:-

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'Richard M. Cheyo'.

Richard M. Cheyo  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
Tume ya Utumishi wa Umma  
17 Juni, 2022